TANGAZO LA SERIKALI NA. 205 la tarehe 28/3/2025

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA)
(SURA YA 287)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 153)*

SHERIA NDOGO YA MAREKEBISHO YA SHERIA NDOGO YA USAFI WA MAZINGIRA YA HALMASHAURI YA WILAYA YA NAMTUMBO YA MWAKA 2025

Jina

TS Na. 270 la 2024

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Marekebisho ya Sheria Ndogo ya Usafi wa Mazingira ya Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo ya Mwaka 2025, na itasomwa pamoja na Sheria Ndogo ya Usafi wa Mazingira ya Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo ya Mwaka 2024 ambayo katika Sheria Ndogo hii inarejewa kama "Sheria Ndogo kuu".

Marekebisho ya kanuni ya 3

2. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika kanuni ya 3-

(a) katika tafsiri ya neno "afisa mwidhiniwa", kwa kuongeza maneno "na Mkurugenzi" mara baada ya neno "atakayeteuliwa"; na
(b) kwa kufuta tafsiri ya msamiati "kaya" na kuiandika upya kama ifuatavyo:
""kaya"maana yake ni familia inayojumuisha baba, mama, mtoto au watoto na mtu mwingine yeyote anayeishi na familia hiyo au watu wanaokaa katika nyumba moja na kuishi kama familia au mtu yeyote anayeishi peke yake katika chumba au nyumba;".

Marekebisho

3. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika kanuni

ya kanuni ya 19

ya 19 kwa kufuta kanuni ndogo ya (2) na kuiandika upya kama ifuatavyo:

> "(2) Kila mkazi mwenye nyumba, mmiliki au mkabidhiwa atapaswa kuweka jengo lake madirisha makubwa kwa vipimo vya madirisha kwa kuzingatia ukubwa wa ukuta au sakafu.".

Marekebisho ya Jedwali la Tatu

4. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika Jedwali la Tatu kwa kufuta neno "ujazo" lililopo katika safu ya pili ya vipengele vya 1 na 2 na badala yake kuweka neno "uzito".

Dodoma,
10 Januari, 2025

MOHAMED OMARY MCHENGERWA,
*Waziri wa Nchi-OR-TAMISEMI*